TANGAZO LA SERIKALI Na. 29 la Tarehe 17/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
SURA YA 287

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

## MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE YA 2025

Jina

TS. Na. 917 la 2023

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale ya Mwaka 2023 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 9

**2.** Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika aya ya 9 kwa kufuta na kuandika upya aya ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

"(3) Kabla ya kuuza mfugo chini ya aya ndogo ya (2), Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio la kuuza mfugo huo.".

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri Wa Nchi- OR-TAMISEMI*